



Ongezeko la Ukimbizi wa Watoto nchini UAE Lahitaji Majibu ya Haraka (Imetafsiriwa)

Habari:

Gazeti la Khaleej Times nchini UAE liliripoti kwamba kuna ongezeko la kutia wasiwasi la watoto wanaokimbia nyumbani. Umri haswa wa vijana hao ni watoto wa kuanzia miaka 7 hadi mabarobaro wachanga. Watoto wengi hupatikana baada ya kuripotija kwa polisi na kabla ya hatari yoyote kubwa kuwajia. Ongezeko la mfadhaiko kutokana na michezo ya kubahatisha mtandaoni, utamaduni wa sinema za watu wazima, mivutano ya wazazi na hofu ya utendaji duni masomoni yote yametajwa kuwa sababu ya matatizo ya watoto na wataalamu.

Habari:

Thaqafa maarufu ya Kiliberali ya Kimagharibi kwa bahati mbaya imeyapiku maadili mema ya ya Kiislamu ambayo yanapaswa kuwa nuru ya uongofu katika nyumba za Waislamu. Dola nyingi za Ghuba zinahalalisha utafutaji wa huduma kwa watoto kutoka kwa wafanyakazi wahamiaji wasiopendezwa kabisa na thaqafa ya maadili ya Uislamu. Ikiwa dori ya mama hatafahamika na kuchukuliwa kuwa kazi ya juu kabisa anayoweza kufanya mwanamke, basi ni jambo lisilokuwa na budi kuwa watoto watapuuzwa kihisia. Wakiachwa kupotoshwa na mawakala wa tabia mbaya na kunyimwa kijamii, watoto wametengwa kisaikolojia kutoka kwa fungamano la malezi ya familia. Kisha wanatolewa nje ya nyumba na kuweza kuhisi kwamba chochote, hata aina nyingine ya mateso, ni bora kuliko maumivu yanayohisiwa mahali ambapo tunapaswa kuwa hifadhi ya usalama. Mwenyezi Mungu (swt) aliweka malipo makubwa na wajibu katika kuchunga kizazi cha mbeleni cha Waislamu kama ilivyojadiliwa katika aya ya Quran;

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوَا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِكُمْ نَارًا وَقُوْدُهَا النَّاسُ وَالْجَاهَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَظٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُمُونَ اللَّهُ مَا أَمْرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمِنُونَ]

“Enyi mlion amini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenge nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrishwa.” [At-Tahrir 66:6]

Kutokana na dalili hii na nyingine nyingi, kina mama wa Kiislamu kamwe wasijihisi kuwa wanaweza kuwepo nyumbani kimwili lakini kutokuwepo kisaikolojia katika malezi ya watoto. Ndani ya Khilafah, shule na nyumba lazima zote zikubalike kwa ajili ya kulea watoto pamoja na msaada wa kijamii. Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt) aurudishe mfumo huu mtukufu kwa mara nyingine tena ili watoto kamwe wasihisi haja ya kukimbia kutoka nyumbani kwao.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na
Imrana Mohammad**